## PESNO II GRADE SEVEN UJUZI WA KUSIKILIZA (KISWAHILI)

**Sikiliza habari ifuatayo ikisomwa na ujibu maswali kwenye karatasi yako ya kujibia**

Busara ni mwanafunzi wa darasa la saba katika shule ya msingi Tumaini. Anaishi na bibi yake katika kijiji cha Mwendokasi. Kijiji hicho kipo karibu na hifadhi ya wanyama ya Mkomazi. Siku moja Jumamosi, Busara na bibi yake walijihimu kulekea shambani. Wakiwa wanakaribia kufika shambani, Busara aliwaona wanyama wawili kwa mbali wakitembea kuelekea upande waliokuwa wakielekea wao. Alimshika bibi yake mkono kwa woga, huku akisema, “bibi! Bibi! Unawaona wale ng’ombe?” bibi aliwaangalia wale wanyama huku akiwa amepigwa na butwaa akamwambia wale si ng’ombe bali ni tembo.